**BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

# HOTUBA YA MWENYEKITI WA KAMATI YA WENYEVITI WA KAMATI ZA KUDUMU ZA BARAZA LA WAWAKILISHI KUHUSU MSWADA WA SHERIA YA FEDHA (USIMAMIZI WA MAPATO) YA MWAKA 2015/16.

**Mheshimiwa Spika,**

Awali ya yote natanguliza shukurani kwa Mwenyezi mungu Mtukufu, kwa kutuwezesha kukutana tena leo hii tukiwa wazima wa afya na kuendelea na kazi hii adhimu ya utumishi kwa wananchi wetu. Nikushuru pia Mheshimiwa Spika kwa kunipa fursa hii kuwasilisha maoni haya kwa niaba ya kamati yangu kuhusu Mswada wa Fedha (Usimamizi wa Mapato) wa mwaka 2015/16.

**Mheshimiwa Spika,**

Mswada huu wa fedha umekuja kwa nia ya kurekebisha sheria mbali mbali za tozo na kodi na kuanzisha tozo nyengine kwa madhumuni ya kuimarisha mapato ya Serikali na udhibiti wake ili kuleta ufanisi mzuri katika utekelezaji wa Sheria hiyo pamoja na kusaidia maendeleo ya wananchi kupita kodi hizo.

**Mheshimiwa Spika,**

Ingawa Mswada huu umeletwa haraka kidogo lakini kamati yangu imekaa na Wizara, na wataalamu wa Sheria wa Serikali na wa Baraza la Wawakilishi ambao wamesaidiana na Kamati katika kuupitia mswada huu na kupendekeza marekebisho mbali mbali ya msingi kwa ajili ya kuufanya Mswada huu uweze kutekelezeka kwa ufanisi.

Mhe Spika, kamati yangu inaiomba afisi yako kwamba ingawa imekaa na Wizara kupitia mswaada wa Fedha lakini tunashauri katika kipindi kijacho basi mswaada huu tuupate mapema ili tupate muda wa kukaa na wadau ili kuweza kupata mawazo yao kwani kuna kodi nyingi hurekebishwa ma walipa kodi wengi hasa wafanyabiashara huwa hawana taarifa au uelewa mzuri katika marekebisho hayo na kuleta usumbufu kwao, lakini pia kuweza kupata mawazo wajumbe wako ili kuweza kuishauri Serikali namna bora ya ukusanyaji kodi Serikalini na kuibua vianzio vipya vya mapato.

**Mheshimiwa Spika,**

Kazi ya kamati ya kuupitia Mswada huu wa Fedha isingekamilika bila ya mashirikiano makubwa niliyopata kutoka kwa wajumbe wa Kamati ambao kwa heshima kuwa naomba niwatambue kama ifuatavyo:-

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Hamza Hassan Juma | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Omar Ali Shehe | Mjumbe |
| 3. | Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Mgeni Hassan Juma | Mjumbe |

5. Mhe. Hija Hassan Hija — Mjumbe
6. Mhe. Mlinde Mabrouk Juma — Mjumbe
7. Mhe. Ussi Jecha Simai — Mjumbe
8. Ndg. Nasra Awadh Salmin — Katibu
9. Ndg. Khamis Hamad Haji — Katibu

**Mheshimiwa Spika,**

Pia nichukuwe fursa hii pia kumshukuru Mheshimiwa , Waziri wa Fedha kwa kuleta Mswada huu lakini pia kwa kushirikiana na kamati katika kuupitia na kutoa ufafanuzi wa hoja mbali mbali za wajumbe akishiriana vizuri na watendaji wake, katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu na watendaji wao mbali mbali.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati imepitia Mswada huu na kupendekeza marekebisho katika vifungu mbali mbali vya Mswada ambavyo havikuwekwa vizuri katika maudhui yake. Katika kifungu cha 4 (1) (a) cha Mswada kamati imependekeza kifungu hicho kiondolewe sehemu ya adhabu ya kifungo na kubakisha adhabu ya faini isiyopungua shilingi hamsini elfu na isiyozidi shilingi laki mbili na hamsini elfu.

Mhe Spika, kamati yangu imeamua kuishauri Serikali kuondoa adhabu ya kifungo na kubakisha adhabu ya fine tu kwasababu kwa kawaida masuala ya biashara ni masuala ya mapatano baina ya mtoza kodi na mtozwa kodi kwa hiyo ni vyema tukaweka adhabu ya fine tu ili kuweka

mazingira mazuri ya Biashara hapa Zanzibar hasa kwa kuzingatia kua Nchi yetu inategemea zaidi uchumi unaotegemea huduma, na ndio maana kukawekwa hata mahakama maalum ya Biashara ( TRADE TRIBUNA) kwa hiyo naomba na wajumbe kutuunga mkono katika kuondoa adhabu hii,na nnaamini kua tutakubaliana katika hili.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati imependekeza marekebisho hayo kwa sababu kifungu hicho cha 4 (1) (a) kinahusu adhabu ya hatia ya kosa kwa Mlipakodi ambaye atashindwa kubandika hati yake ya usajili ya Mlipakodi katika sehemu inayoonekana. Kamati imeona kuwa si busara kuweka adhabu ya kifungo kwa kosa hilo kwa Mlipakodi kwa kosa ambalo athari yake siyo kubwa sana. Vile vile kamati imefikiria pia si busara kuweka adhabu za vifungo kwa walipakodi pale ambao hakuna ulazima wa kufanya hivyo.

**Mheshimiwa Spika,**

Katika kifungu cha 11 cha Mswada huu kinachohusu kuwekwa kwa kifungu kipya cha 53 A, kwenye maneno ya proviso kamati imefanya marekebisho madogo ya kuongeza neno **"kama ushahidi"** baaada ya neno "itakubaliwa". Sababu ya kuongezwa maneno hayo ni kuwezesha maudhui ya proviso hiyo yaende sambamba na maelezo yaliyotangulia yanayohusu taarifa au nyaraka yoyote ya mlipakodi itakayopatikana na Afisa anayehusika na kodi kutumika kama ushahidi katika uendeshaji

wa mashauri yoyote kulingana na kosa au madai ya kodi chini ya sheria hiyo ua sheria nyengine inayosimamiwa na Bodi ya Mapato.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati ilipokuwa inaupitia Mswada huo, imependekeza mpangilio mpya wa nambari za vifungu. Kifungu cha 12 cha Mswada kinachorekebisha kifungu cha 54A cha Sheria mama kimefutwa na kamati imependekeza kuwa kifungu cha 13 cha Mswada sasa kitakuwa cha 12 na vifungu vyengine vitafuta mpangilio huo.

**Mheshimiwa Spika,**

Marekebisho mengine yaliyopendekezwa na Kamati yanahusu mlingano wa vifungu katika nakala ya Mswada wa kingereza na Kiswahili. Katika kifungu cha 21 (3), kwenye orodha ya vyanzo vya kodi za Miundombinu, kamati inapendekeza kuwekwa kwa kodi ya Uingizaji bidhaa kutoka nje ya Zanzibar ambayo itatozwa kwa asilimia 60% ya makusanyo. Maneno hayo yanaonekana katika nakala ya Kingereza peke yake.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inapendekeza pia kuongezwa kwa kifungu kipya cha 22 ambacho kitasomeka kama kinavyoonekana katika ukurasa wa 3 wa nakala ya marekebisho ya kamati iliyosambwazwa kwa wajumbe wote.

**Mheshimiwa Spika,**

Wakati kamati inapitia Mswada huu kulikuwa na mjadala katika kifungu cha 21 kuhusu kuanzishwa kodi ya Miundombinu ambayo kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (3) cha kifungu hicho, kodi hiyo itahusisha vianzio katika malazi ya wageni katika hoteli zilizopo Zanzibar, wasafiri kutoka bandari yoyote ya Zanzibar kwenda katika bandari nyengine ndani  na nje ya Zanzibar, kodi ya abiria anayeondoka kupitia uwanja wa ndege na kuelekea sehemu yoyote ya Tanzania, kodi ya bidhaa za petrol na deseli na mauzo ya umeme.

**Mheshimiwa Spika,**

Hoja mbali mbali za wajumbe zilizoibuka kutokana na kuanzishwa kodi hiyo ya miundombinu katika vianzio hivyo, zimekuja kwa nia ya kamati kutaka kuhakikishiwa kuwa kodi hizo hazitakuwa mzigo kwa mwananchi wa kawaida na badala yake zinasaidia katika maendeleo ya wananchi wenyewe.

**Mheshimiwa Spika,**

Katika kodi ya 2% ya mauzo ya umeme, kama inavyoonekana katika kifungu hicho cha 21 (3), kamati ilikuwa na wasiwasi kuwa huenda ikaongeza gharama za matumizi ya umeme kwa mwananchi wa kawaida. Naomba niwatoe wasiwasi wananchi kuwa ongezeko hilo halitahusu kwa kila unit moja ya umme anayotumia mwananchi, badala yake itatozwa kutoka katika gharama za jumla za mauzo.

**Mheshimiwa spika,**

Mwananchi yoyote atakayenunua umeme wa shilingi elfu tano atalazimika kulipa 2% ya mauzo hayo ambayo ni shilingi mia moja. Sehemu kubwa ya kodi hiyo itaelekezwa katika maeneo mengine ya kuimarisha huduma za jamii katika miundombinu.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati yangu haina tatizo tena na kuanzishwa kwa chanzo hicho cha kodi katika kodi ya Miundombinu, isipokuwa nasisitiza kuwa kila mtu anayetumia huduma ya umeme atalazimika kulipa kodi hiyo. Kumekuwa na utamaduni usio sahihi katika mashirika mengi ya umma ambayo yanatoa huduma ambazo wananchi huzilipia lakini huduma hizo nyengine hutolewa bure kwa watendaji wa mashirika hayo.

**Mheshimiwa spika,**

Kamati yangu inatoa angalizo kwa Serikali kuwa mashirika ya umma siyo sadaka, yanapotoa huduma zake lazima huduma hizo zilipiwe na faida ipatikane kwa Serikali. Kamati yangu inataka Serikali kuhakikisha watendaji wa Shirika la Umeme wote wanalipa huduma ya umeme na kodi ya mauzo ya 2% iliyowekwa ihakikishwe inalipwa kutoka na mauzo hayo.

**Mheshimiwa Spika,**

Baada ya ufafanuzi wa kina wa hoja mbali mbali zilizoibuka wakati wa kupita mswada huu, Kamati yangu imeridhika na Mswada huu, tunamtaka Mheshimiwa Waziri kukubaliana na mapendekezo ya marekebisho ya mswada kama yanavyooneaka na katika waraka wa marekebisho wa kamati ambao umegawiwa kwa wajumbe.

**Mheshimiwa Spika,**

**Mambo ya kijumla katika mswaada wa Sheria hii.**

Kimsingi kamati yangu inaunga mkono marekebisho na mapendekezo yote ya Sheria mbali mbali za kodi ili kuweza kumpa mamlaka Waziri kuweza kuwa na maamuzi sahihi kwa mujibu wa Sheria, lakini bado kamati yangu inaishauri Serikali kua wakati umefika kutafuta vianzio vipya vya uhakika vya mapato aidha kuharakisha Program ya PPP ili kupata makampuni ambayo yataingia ubia na Serikali, na kuweza kuzalisha mali au kutoa huduma zitakazo kua na tija zaidi, lakini pia Serikali kuharakisha mpango wa kuanzisha mradi wa uvuvi wa Bahari kuu ili kuweza kutoa ajira kwa vijana wetu, pia kuweza kupata mapato yatakayotokana na mauzo ya Samamaki hao, lakini jingine na kwamba tukianzisha uvuvi wa Bahari kuu basi pia tuanzishe viwanda vya kusindika samaki ili kuweza kua na kitoweo cha kutosha pamoja na kuuza nje jambo ambalo linaweza kutuletea pesa za kigeni, na kupunguza nakisi ya uingizaji na usafirishaji wa bidhaa nje ya nchi.

Kwa hiyo tunaiomba Serikali kutafuta kampuni zenye uwezo ili kuja kuekeza katika sekta hizo na tunaamini zipo nyingi Duniani.

**Mhe Spika,** kamati yangu bado tunaendelea kuishauri Serikali kuangalia uwezekano wa kuanza kuzisarifu Karafuu zetu ili kuondokana na kziuza kama zilivo kwenye maguni ajambo ambalo linaikosesha sana Serikali mapatona ajira kwa kiasi kikubwa, kwani tunaamini karafuu na mwani kama utasarifiwa hapahapa Zanzibar basi zitaweza kuongeza mapato kwa kiasi kikubwa.

Mhe Spika, kwa kua katika marekebisho haya ya kodi kuna tozo ya asilimia mbili kwa watumiaji wa umeme basi wananchi wangelipenda kujua hiyo asilimia ya kodi itakua kwa kila Unit au kwa kila mauzo? Lakini pia je tozo ya kodi hiyo itamsaidia nini mwananchi katika kuboresha huduma zake za maisha ya kila siku?.

**Mhe Spika,** kamati yangu inaitaka Serikali kila inapotaka kuongeza au kutoza kodi mpya basi wawe na utamaduni wa kuwaelezea wananchi kupitia vyombo vya Habari namna kodi hiyo itakavyoenda kutumika na faida gani wataweza kuipata kupitia kodi hiyo nnaamini kua wananchi wakijua tu basi hawatakua wagumu katika kuchangia kodi hiyo kwani tumejifunza nchi za Ulaya na Uingereza hata wanapotaka kuongeza ada kwenye usafiri basi ndani ya vyombo hivyo vya usafiri utasikia matangazo kua kuanzia mwezi Fulani bei ya Ticket ya Train itaongezeka kwa kiasi Fulani kwasababu aidha wanataka kuboresha baadhi ya

huduma au kuimarisha miundombinu ya usafiri , kwa hiyo wananchi hupata kujua taarifa hiyo mapema na wanajua ikifika muda huo basi bei ya Ticket hiyo itaongezeka kwa kiasi gani, na mara nyingi hujipanga hata katika bajet zao binafsi za matumizi.

**Mhe Spika,** kama nilivyoelezea katika hotuba yangu ya ripoti ya kamati ya Wenyeviti kuhusu Bajet kuu ya Serikali kwenye ada ya Bandari ambayo pesa zake zinaenda moja kwa moja kwenye ununuzi wa madawati basi kuwe na uangalizi maalum wa matumizi ya pesa hizo vinginevyo tatizo la madawati linaweza kua ni mradi wa baadhi ya watu kutaka kujinufaisha wao wenyewe, Lakini pia kamati yangu inaishauri Serikali kupitia wizara ya Elimu kuweza pia kuzitumia pesa hizo za kuyakarabati baadhi ya Madeski yaliyoharibika ili kuokoa pesa nyingi za kuchongas madawati mapya kamati yangu tunaamini kua ikiwa yatakusanywa kufanyiwa ukarabati basi yataweza kuokoa kiasi kikubwa cha pesa hizo kwani yapo mengi sana ambayo yanaweza kutengenezeka.

**Mhe Spika,** kuhusu kodi ya Miundombinu tunamtaka Waziri anaeshughulikia masuala ya Fedha kuandaa kanuni kwa haraka itakayoweza kuweka Utaratibu maalum wa matumizi na mgawanyo wa pesa hizo ili ziweze aidha kuisaidia mifuko mingine au kutoa ufanisi mzuri kama ilivyokusudiwa vinginevyo inaweza pia kodi hii pia ukawa mradi wa watu wachache wa kujinufaisha wenywe, kwani tunaamini mfuko huu utawezaweza kuisaidia na kuisukuma miradi na mifuko mingine kama ilivyokusudiwa. Na nnaamini kama kweli ada hii ya

miundombinu kama tulivyoelezwa basi itaweza kuondoa mambo mengi madogomadogo na yale ya dharura.

**Mhe Spika,**

Nikushukuru tena kunipa fursa hii ya kuwasilisha maoni haya, kwa niaba ya kamati na kwa vile Mswada huu siyo mkubwa, na Mheshimiwa Waziri ametoa maelezo ya kina ya ufafanuzi, kamati yangu inaukubali na nawaomba waheshimiwa wajumbe waujadili, watowe maoni yao kwa nia ya kurekebisha, kuimarisha na hatimaye kuupitisha, ili kumuwezesha Mheshimiwa Waziri akakusanye fedha kwa ajili ya kuwahudumia wananchi katika mwaka huu wa Fedha 2015/2016.

Mheshimiwa Spika, Nakushukura na naunga mkono hoja.

……………………

Mhe. Hamza Hassan Juma,

Mwenyekiti,

Kamati ya Wenyeviti wa Kamati za Kudumu,

Baraza la Wawakilishi,

# Zanzibar.